GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6649 **20 Aprili, 2017** **Bei, Shs. 3000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa n i Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo..... 107

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 10 Mei, 2017 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza, na unachapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
20 Aprili, 2017

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa. Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa
SHERIA YA KUANZISHA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara ya 2017 na itaanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika kwa Sekta ya Umma na Sekta binafsi kwa ajili ya Jukwaa la biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo-

" Sheria" maana yake ni Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara;

"Mwenyekiti wa Baraza" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Jumuiya" maana yake ni jumuiya ya wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima Zanzibar;

"Kamati" maana yake ni Kamati za Baraza zilizoanzishwa chini ya kifungu cha 17 cha Sheria hii;

"Baraza" maana yake ni Baraza liloanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii;

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji wa Baraza aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11 (1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na Biashara;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Kamati Tendaji" maana yake ni Kamati Tendaji iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 14 cha Sheria hii.

Malengo ya Baraza.

4. Baraza la Taifa la Biashara lina malengo yafuatayo-

(a) kuandaa mikutano au majadiliano baina ya sekta za Umma na sekta Binafsi kwa dhamira ya kupata muafaka na uwelewa juu ya mambo ya msingi yanayohusiana na usimamizi na ukuaji wa uchumi;

(b) kuzidisha ukuaji wa uchumi kwa lengo la kupunguza umaskini na kuendeleza maendeleo endelevu;

(c) kutathmini muda baada ya muda maendeleo ya nje na mazingira ya kibiashara ya ndani, changamoto, na fursa kwa lengo la kupata suluhisho;

(d) kubadilishana uzoefu juu ya utekelezaji uliokuwepo na mazingira yakurekebishwa kwa lengo la kuboresha utendaji mzuri wa biashara na utoaji wa huduma;

(e) kutathmini na kupendekeza uboreshaji wa sera za kimazingira ambazo zitawavutia Wawekezaji na ushindani wa kibiashara; na

(f) kuzingatia jambo jengine lolote ambalo litapelekea kwa Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC) kufikia malengo yake.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI WA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR

Uanzishwaji wa Baraza.

5.-(1) Kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Biashara kwa ufupi litajulikana kama (ZNBC).

(2) Baraza litakuwa ni jukwaa la majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Muhuri wa Baraza.

6.-(1) Kutakuwa na Muhuri wa Baraza ambao umbo na ukubwa wake utapendekezwa na kamati tendaji wa kuamuliwa na Baraza.

(2) Matumizi ya Muhuri wa Baraza juu ya nyaraka yoyote itathibitishwa na saini ya Katibu Mtendaji au afisa mwengine yoyote wa Baraza aliyeidhinishwa na Katibu Mtendaji.

(3) Nyaraka yoyote itakayotolewa na Baraza ili ijulikane kuwa ni hati rasmi iliyotolewa na Baraza itatakiwa iwe imepigwa muhuri wa Baraza na imethibitishwa kwa mujibu wa kifungu cha (2) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa ni hati rasmi ya Baraza na itapokelewa kama ushahidi bila uthibitisho mwengine wowote.

Muundo wa Baraza.

7.-(1) Baraza litajumuishwa na wajumbe wafuatao-

(a) Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mawaziri kutoka wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

(c) Wajumbe kumi na mbili kutoka sekta binafsi;

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) (b) na (c) cha kifungu hiki, uwiano wa Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta ya Umma na sekta binafsi utakuwa sawa.

(3) Mwenyekiti anaweza kumualika mtu yoyote mwenye weledi kutoka sekta ya umma au sekta binafsi kuhudhuria mkutano wa Baraza ili kutoa mchango wa ujuzi wake kama Mwenyekiti atakapoona inahitajika.

Uteuzi wa wajumbe wa Baraza

8.-(1) Mwenyekiti ana uwezo wa kuteua wajumbe wa Baraza kama ifuatavyo:

(a) Mawaziri kutoka Wizara tofauti kama atakavyoona inafaa;

(b) Wakuu wa jumuiya za sekta binafsi ambao watateuliwa kutoka jumuiya ya wafanyabiashara, viwanda na wakulima na wajumbe wengine si wanachama wa Jumuiya hii.

(2) Katika kuteua wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) cha Kifungu hiki, Rais atalazimika kushauriana na jumuiya ya wafanyabiashara.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Rais atazingatia jinsia katika kuteua wajumbe kutoka sekta binafsi.

(4) Wajumbe kutoka sekta binafsi watatoka sekta ikijumuisha biashara, fedha, viwanda, utalii, kilimo na uvuvi, uchimbaji madini, usafiri na mawasiliano, elimu , afya, ujenzi na ufundi na sekta nyengine za biashara.

(5) Mwenyekiti wa Baraza baada ya kupokea mapendekezo na kujadiliana na sekta binafsi anaweza kumuondoa mjumbe na kujaza nafasi kwa mjumbe yoyote kutoka sekta binafsi.

Kazi za Baraza.

9. Kazi za Baraza zitakuwa ni-

(a) kukuza mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi

(b) kuweka utaratibu wa majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi;

(c) kuyapitia mambo yanayoanzia katika mikutano au majadiliano yanayohusiana na maendeleo ya kiuchumi na kushauri njia sahihi za utatuaji kwa utekelezaji kwa sekta husika;

(d) kufanywa au kusababisha kufanywa kwa utafiti, ukaguzi au mafunzo juu ya sera za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kama Baraza litakavyoona inafaa;

(e) kupitia utekelezaji wa maazimio ya Baraza kwa sekta inayohusika;

(f) kupokea, kuyapitia na kutoa mapendekezo juu sera, utafiti, taarifa au ushauri uliowasilishwa kwenye Baraza unaohusiana na biashara na maendeleo ya kiuchumi;

(g) kuweka malengo pamoja na muda wa utekelezaji wake kwa utekelezaji wa miongozo, maamuzi au maazimio ya Baraza;

(h) kusimamia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Baraza;

(i) kupokea na kuipitia taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya Baraza na kutoa muongozo au ushauri;

(j) kuwa na uhusiano au ushirikiano na Mabaraza mengine ya biashara kwa lengo la kutafuta ujuzi na kubadilishana taarifa;

(k) kuanzisha Kamati endapo itahitajika kwa utekelezaji wa kazi za Baraza;

(l) kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Baraza la Mkoa kwa ajili ya kuiidhinisha ; na

(m) kufanya kazi nyengine yoyote kwa madhumuni ya kukuza mazingira ya biashara na maendeleo ya uchumi.

(2) Baraza linaweza ikiwa litaona inafaa kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati au Katibu Mtendaji au Baraza la Mkoa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Baraza.

Mikutano na jukwaa la majadiliano la Baraza.

10. Mikutano ya Baraza, akidi, maazimio majadiliano litalazimika kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Katibu Mtendaji.

11.-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji ambae atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji ikiwa ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya utawala, wa umma uongozi wa usimamizi wa biashara, sheria, uchumi na fani nyengine zinazofanana na hizo kutoka chuo kinachotambulika na uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano.

(3) Kwa madhumuni ya Sheria hii, Katibu Mtendaji atakuwa na jukumu la kusimamia, kuratibu mambo yote yanayohusiana na uongozi na shughuli za kila siku za Baraza.

(4) Katibu Mtendaji atakuwa anawajibika katika kutekeleza majukumu ya kazi zake kama atakavyoelekezwa na Baraza au Kamati Tendaji.

Majukumu ya Katibu Mtendaji.

12.-(1) Katibu Mtendaji atatekeleza majukumu yafuatayo-

(a) kutekeleza kazi za kila siku za Baraza;

(b) kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza pamoja na Kamati zake;

(c) kutayarisha hoja zinazotakiwa kujadiliwa katika vikao vya Baraza, Kamati Tendaji na Kamati mbalimbali za Baraza;

(d) kufatilia utekelezaji wa maazimio ya Baraza;

(e) kuratibu shughuli za Mabaraza ya Mikoa;

(f) kutayarisha bajeti ya kila mwaka ya kazi za Baraza na kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji kwa ajili ya kuthibitishwa;

(g) kuandaa mpango mkakati wa kibiashara wa Baraza;

(h) kutayarisha ripoti ya utekelezaji kazi za Baraza; na Baraza au

(i) kufanya kazi nyengine yoyote atakayoelekezwa na Kamati Tendaji.

(2) Katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki, Katibu Mtendaji atakuwa chini ya usimamizi na miongozo ya Wazara ya Biashara.

(3) Kwa kuzingatia Kifungu kidogo cha(1) cha Kifungu hiki,Katibu Mtendaji atafuata, maelekezo au miongozo atakayopewa na Baraza.

Wafanyakazi wa Baraza.

13.-(1) Katibu mtendaji baada ya idhini ya Kamati Tendaji anaweza anaweza kuajiri wafanyakazi kwa idadi ambayo ataona inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wafanyakazi walioajiriwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watakuwa chini ya udhibiti na usimamizi wa Katibu Mtendaji.

SEHEMU YA TATU
UANZISHWAJI NA MUUNDO WA KAMATI YA BARAZA

Uanzishwaji wa Kamati Tendaji.

14. Kutakuwa na Kamati Tendaji ya Baraza.

Muundo wa Kamati Tendaji.

15.-(1) Kamati Tendaji itajumuisha wajumbe kumi ambao watakuwa na uwakilishi sawa kutoka sekta ya umma na sekta binafsi kama ifuatavyo;

(a) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mwenyekiti mwenza ambaye atateuliwa na Kamati Tendaji kutoka miongoni mwa wajumbe wa sekta binafsi;

(c) Wajumbe kutoka sekta ya umma watateuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi kama atakavyoona inafaa; na

(d) Wajumbe kutoka sekta binafsi watakuwa ni maafisa waandamizi watakaowakilisha jumuiya zao na watatoka kutoka jumuiya ya wafanyabiashara, viwanda na wakulima, chama cha wafanyakazi,wawekezaji wa utalii, usafirishaji wa bahari, na jumuiya zisizokuwa za kiserikali.

(2) Katika kuteua wajumbe kutoka sekta binafsi, jumuiya ya wafanyabiashara na jumuiya nyengine amabazo si wanachama wa jumuiya ya wafanyabiashara watawasilisha majina wanayoyapendekeza kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya uteuzi.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa katibu wa Kamati Tendaji.

(4) Bila kuathiri muundo wa Kamati Tendaji, wajumbe kutoka sekta binafsi wanaweza kubadilishwa na Kamati Tendaji kama itakavyoona inafaa.

Kazi za kamati Tendaji.

16. Kazi za Kamati Tendaji zitakuwa ni:

(a) kushughulikia ufanyikaji wa vikao vya Baraza;

(b) kuandaa ajenda za mkutano wa Baraza

(c) kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maamuzi ya Baraza;

(d) kuangalia kazi za Katibu Mtendaji wa Baraza kwa ajili ya kuhakiisha malengo yaliyokusudiwa yamefikiwa;

(e) kuandaa utaratibu na itifaki kwa ajili ya kushughulika na kufikiwa kwa maamuzi na makubaliano ya Baraza ikijumjuisha kuratibu na utekelezaji wa maazimio ya Baraza;

(f) kusaidia kufanyika kwa vikao vya kamati za Baraza;

(g) kuthibitisha bajeti ya mwaka, mpango kazi na masuala ya ajira na kuwasilisha kwa wizara ya biashara, viwanda na masoko kwa taarifa. na kuiwasilisha katika Baraza kwa taarifa;

(h) kurahisisha utekelezaji wa kazi za Baraza;

(i) kusimami uongozi na utawala wa Baraza;

(j) kuanzishwa muundo wa taasisi na utaratibu wa kutekeleza kazi za Baraza kama itakavyoonekana inafaa;

(k) kuanzisha kamati ikiwa ni miongoni mwa wajumbe wake au vyenginevyo, ambaye atakasimiwa uwezo huo kama itakavyoonekana inafaa;

(l) kuthibitisha mpango wa utekelezaji, malengo na mpango mkakati wa biashara kwa kamati na kuratibu utekelezaji wake kwa ajili ya kuhakikisha unafikia malengo endelevu;

(m) kutekeleza jukumu jengine lolote watakalopewa chini ya Sheria hii au maelekezo ya Baraza.

Mkutano wa Kamati Tendaji

17. Mkutano, akidi na maamuzi ya Kamati Tendaji yatafanywa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la pili la Sheria hii.

SEHEMU YA NNE
UANZISHWAJI WA KAMATI ZA BARAZA

Kamati za Baraza.

18.-(1) Kutakuwa na Kamati zitakazoanzishwa na Baraza kama itavyoona inafaa.

(2) Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki zitakuwa na uwezo wa kutekeleza jambo lolote watakalopewa na Baraza, Taasisi ya kibiashara ya kijamii au mtu yoyote mwenye maslahi nalo.

(3) Baraza litakuwa na Kamati zifuatazo-

(a) Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi;

(b) Kamati ya Utalii;

(c) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; na

(d) Kamati ya mambo ya Ajira.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Bodi inaweza kuanzisha Kamati nyengine yoyote kama itavyoona inafaa kwa utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

(5) Wajumbe wa Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, watakuwa kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la pili la Sheria hii.

(6) Kwa kuzingatia miongozo na maelekezo itakayotolewa na Baraza, Kamati zinaweza kuweka utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zake zenyewe.

Kumualika mtu.

19. Kamati zinaweza kumualika mtu yeyote mwenye utalamu mahsusi kuhudhuria na kushiriki katika majadiliano ya kamati kwa ajili ya kutoa ushauri kwa kamati hiyo juu ya jambo lililojadiliwa, lakini mtu huyo aliyoalikwa hana uwezo wa kupiga kura.

Kazi za Kamati.

20. Kila Kamati ya Baraza itakuwa na kazi zake kama zifuatazo:

(a) Kamati ya uchumi, biashara uwekezaji na kodi ina wajibu wa-

(i) kuwezesha utekelezaji wa maamuzi ya Baraza au Jukwaa la Biashara

(ii) kupokea jambo lolote au lalamiko linalohusiana na Jukwaa la bishara kutoka kwa mtu yoyote ;

(iii) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yatakayosaidia kukuza uchumi endelevu;

(iv) kupendekeza namna ya kuimarisha mazingira mazuri ya kibiashara, viwanda na uwekezaji;

(v) kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya biashara, viwanda na uwekezaji;

(vi) Kuimarisha ukusanyaji wa kodi na mapato;

(vii) kuainisha matatizo yanayoikali mfumo wa kodi na kuyatatuai;

(viii) kuimarisha fursa za uwekezaji kwa mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi; na

(ix) kutekeleza jambo jengine lolote watakaloelekezwa na Baraza.

(b) Kamati ya utalii ina wajibu wa-

(i) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yatakayosaidia kukuza sekta ya utalii;

(ii) kuainisha matatizo yanayoikabili sekta ya utalii-Zanzibar;

(iii) kupendekeza hatua za kutatua matatizo ya sekta ya utalii;

(iv) kupendekeza hatua za kuimarisha skta ya utalii;

(v) kuwezesha utekelezaji wa Baraza; na

(vi) kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(c) Kamati ya kilimo, ufugaji na uvuvi ina wajibu wa-

(i) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbaliyanayohusiana na maendeleo katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi;

(ii) kuainisha matatizo yanayoikabili sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi;

(iii) kuwezesha utekelezaji wa maamuzi ya Baraza

(iv) kupendekeza hatua za kutatua matatizo yote katika sekta hii; na

(v) kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(d) Kamati ya Ajira inawajibu wa-

(i) kuanisha fursa za ajira;

(ii) Kutatua matatizo ya wafanyakazi; na

(iii) kuainisha matatizo ya wafanyakazi kupendekeza hatua za kuyatatua;

(iv) kuwezesha utekelezaji wa maamuzi ya Baraza; na

(v) Kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(2) Baraza linaweza kuongeza idadi ya kamati nyengine au kuzibadilisha wajumbe wa kamati hizo, pale itakapoona inafaa.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa ni Katibu wa Kamati.

(4) Katibu Mkuu Kiongozi atawajuilisha kwa maandishi wajumbe watakaouteuliwa kuwa wajumbe wa kamati mbalimbali.

(5) Kamati zitawasilisha taarifa za utekelezaji kwa ajili ya kuidhinishwa kama itakavyohitajika na Baraza ndani ya muda utakaoamuliwa na Katibu Mtendaji.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MABARAZA YA MIKOA

Muundo wa Baraza la Mkoa.

21.-(1) Kutakuwa na Baraza la Mkoa kwa kila Mkoa ambalo litakuwa na wajibu wa kutekeleza kazi za Baraza zilizokasimiwa kwa Baraza la Mkoa husika.

(2) Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mkoa.

(3) Baraza la Mkoa linaundwa na wajumbe kumi na mbili, sita kutoka sekta ya umma na sita kutoka sekta binafsi.

(4) Wajumbe wa Baraza la Mkoa kutoka sekta ya umma watateuliwa na Mkuu wa Mkoa kwa kushauriana na Taasisi za umma husika.

(5) Wajumbe kutoka sekta binafsi wataeuliwa na Mkuu wa Mkoa kwa kushauriana na Taasisi binafsi katika Mkoa husika.

(6) Katibu Tawala wa Mkoa atakuwa Katibu wa Baraza la Mkoa

Kazi za Baraza la Mkoa.

22. Baraza la Mkoa lina kazi zifuatazo:

(a) kutekeleza maamuzi ya Baraza;

(b) kupeleka mapendekezo ya kibiashara kwa Baraza;

(c) kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Baraza;

(d) kuwasiliana na Katibu mtendaji kwa jambo lolote lililo jitokeza linalohusiana na biashara kwa ajili ya kufanyiwa kazi na kulitatua;

(e) kuandaa jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi ya Mkoa;

(f) kupokea na kuzingatia mambo yote yanayohusiana na ukuzaji wa biashara na maendeleo ya uchumi katika ngazi ya Mkoa na kupendekeza njia muafaka;

(g) kujadili na kutafuta suluhisho kuhusiana na maendeleo ya biashara katika ngazi ya mkoa; na

(h) kutekeleza jambo jengine lolote kama watakavyoelekezwa na Baraza.

Wajibu wa Baraza la Mkoa.

23.-(1) Baraza la Mkoa lina wajibu wa kusaidia utekelezji wa kazi za Baraza katika ngazi husika ya Mkoa kwa ajili ya kuhakikisha jukwaa la majadiliano kuhusiana na masuali ya biashara baina ya Serikali na sekta binafsi linafanikiwa.

(2) Baraza la Mkoa linatekeleza kazi zake chini ya usimamizi na maelekezo ya Baraza.

(3) Baraza la Mkoa litakutana katika vikao vyake vya kawaida angalau mara mbili kwa kila mwaka, lakini linaweza kuitisha kikao cha dharura wakati wowote kadri hali itakapohitajika.

(4) Baraza la Mkoa linaweza kuanzisha kamati mbali mbali za kutekeleza kazi, pale itakapoona inafaa, kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi za Baraza katika ngazi ya Mkoa husika.

(5) Baraza la Mkoa litaweka na kuhifadhi kumbukumbu za kila kikao na litatayarisha ripoti ya utekelezaji na kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji ya Baraza, ripoti yamwaka itajumuisha-

(a) utekelezaji wa kazi na shughuli za Baraza la Mkoa;

(b) utekelezaji wa maelekezo ya Baraza;

(c) mapato na matumizi;

(d) kupendekeza mapendekezo juu ya kuimarisha maendeleo ya biashara katika ngazi ya Mkoa husika; na

(e) kutekeleza kazi nyengine yoyote inayohusiana na biashara katika ngazi ya Mkoa.

(6) Vyanzo vya fedha vya Baraza la Mkoa vitatoka Baraza la Taifa la biashara.

SEHEMU YA SITA
UANZISHWAJI WA JUKWAA LA BIASHARA

Kuanzishwa kwa Jukwaa la biashara Kuanzishwa kwa Jukwaa la biashara.

24.-(1) Kutakuwa na Jukwaa la Biashara la Baraza ambalo litakuwa na muundo ufuatao:

(a) Mwenyekiti wa Baraza ;

(b) Wajumbe wa Baraza;

(c) Wajumbe wa Baraza la Mkoa;

(d) Wajumbe kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara;

(e) Wajumbe kutoka jumuiya nyengine za kibiashara; na

(f) Wafanyabiashara wengine kama Baraza litakavyoamua.

(2) Baraza litaandaa Jukwaa la biashar baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kukuza mashirikiano na majadiliano.

(3) Jukwaa la biashara litafanywa mara moja kwa kila mwaka, lakini linaweza kufanyika itakapohitajika.

(4) Baraza linaweza kumwalika mtu yoyote kuhudhuria Jukwaa la biashara.

(5) Jukwaa la biashara litapokea, kujadili , na kutoa mapendekezo juu ya mambo yaliyowasilishwa mbele ya Baraza.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha.

25.-(1) Kutakuwa na vyanzo vya fedha vya Braza ambavyo vitajumuisha:

(a) Fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya Baraza

(b) michango kutoka sekta binafsi; na

(c) Fedha zilizopatikana kwa njia za halali ambazo zitalipwa au kuingizwa kwa Baraza chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Mwaka wa fedha wa Baraza utaanza siku ya mwanzo ya Julai na kumalizika siku ya mwisho ya Juni ya mwaka unaofuata.

Makadirio ya mwaka.

26.-(1) Angalau miezi mitatu kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, Katibu Mtendaji atatayarisha, makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka ya Baraza kwa ajili ya mwaka unaofuata

(2) Katibu Mtendaji kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Kamati Tendaji makadirio mapato na matumizi ya mwaka kwa ajili ya kuidhinishwa.

Hesabu za ukaguzi.

27.-(1) Baraza litalazimika kusimamia vitabu vya hesabu na kumbukumbu za risiti za matumizi.

(2) Vitabu vya hesabu na kumbukumbu za fedha za Baraza zitahifadhiwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria ya Usimamizi wa fedha za umma na Kanuni zake.

(3) Vitabu vya hesabu vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali au mtu mwengine yeyote aliyemuidhinisha na vitakaguliwa angalau kila mwisho wa mwaka wa fedha.

(4) Hesabu zilizokaguliwa na ripoti ya Mkaguzi zitawasilishwa katika Baraza sio chini ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha.

(5) Katibu Mtendaji analazimika baada ya kupokea ripoti kutoka kwa mkaguzi kuiwasilisha Kamati Tendaji.

(6) Katibu Mtendaji analazimika, kumpa taarifa zote Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali na kumwezesha kuweza kufanya ukaguzi.

(7) Katibu Mtendaji analazimika kuiwasilisha ripoti ya mwaka kwa wasimamizi wa fedha kwa maka huo wa fedha, pamoja na maelezo ya fedha ya fedha kwa Kamati simamizi na Waziri kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa fedha za umma.

(8) Matumizi yoyote ya Baraza yatafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake.

SEHEMU YA NANE
MASHARFTI MENGINEYO

Kanuni.

28. Waziri anaweza, kwa kushauriana na Kamati Tendaji kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza

29.-(1) Tangazo la Kisheria Namba. 106 of 2011 linafutwa.

(2) Jambo lolote lililofanywa au hatua yoyote iliyochukuliwa au iliyofanywa chini ya Tangazo la Kisheria lililofutwa chini ya Kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki, litachukuliwa kwamba limefanywa au kutekelezwa chini ya masharti ya Sheria hii.

JADWELI LA KWANZA

UTARATIBU WA UENDESHAJI WA VIKAO VYA BARAZA
[Chini ya Kifungu cha 10]

Vikao vya Baraza.

1.-(1) Baraza litafanya vikao vyake angalau mara moja kwa mwaka, lakini wanaweza kufanya kikao chengine cha dharura wakati wowote, pale litakapoona inafaa.

(2) Akidi ya vikao vya Baraza itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria kikao na angalau asilimia arubaini 40% ya wajumbe watoke katika sekta zote mbili, sekta ya umm ana sekta binafsi.

(3) Vikao vyote vya Baraza vitaongozwa na Mwenyekiti.

(4) Endapo kwa maoni ya Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Baraza, ikiwa kuna jambo linaonekana ni la haraka na la dharura haliwezi kusubiri utaratibu wa kuja kujadiliwa katika vikao vya Baraza, jambo hilo linaweza kujadiliwa na kutolewa maamuzi katika ngazi ya kamati

(5) Maamuzi yaliyofikiwa chini ya Kifungu kidogo cha (4) cha Kifungu hiki, yatakuwa ni halali na yenye nguvu na yatatolewa ufafanuzi na kuwasilisha taarifa yake katika Baraa kwa ajili ya mazingatio na kuthibitishwa.

(6) Maamuzi ya Baraza kwa jambo lolote liloletwa kwa kufanyiwa maamuzi yatafanywa kwa kufikia maamuzi yapamoja.

(7) Baraza linaweza kumwalika mtu yoyote kuja kutolea ufafanuzi jambo lolote wakati wa mkutano, lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

JADWELI LA PILI
UTARATIBU WA UENDESHAJI VIKAO VYA KAMATI TENDAJI
[Chini ya Kifungu cha 17]

1. Kamati Tendaji itafanya vikao vyake vya kawaida angalau mara mbili kwa mwaka na inaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote pale inapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake sehemu yoyote kama itakavyoamuliwa na Kamati Tendaji.

2. Vikao vyote vya Kamti Tendaji vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa Mwenyekiti hayupo Makamu Mwenyekiti kutoka jumuiya ya wafanyabiashara, viwanda na wakulima ataendesha kikao hicho.

3. Wajumbe wa Kamati Tendaji watamteuwa mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makmu Mwenyekiti.

4. Akidi ya vikao vya Kamati Tendaji itapatikana kwa zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka sekta ya umma na sekta binafsi.

5. Maamuzi ya Kamati Tendaji yatapatikana kwa maridhiwano ya wajumbe waliohudhuria kikao.

JADWELI LA TATU

WAJUMBE WA KAMATI ZA BARAZA

[Chini yakifungu cha 18(5)]

5.-(1) Muundo wa wajumbe wa Kamati utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kamati ya uchumi, biashara, uwekezaji na kodi.

(i) Waziri mwenye dhamana na Biashara ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri wa Fedha;

(iii) Waziri wa Ardhi;

(iv) Waziri kutoka Afisi ya Makamu wa Pili;

(v) Katibu Mkuu , kutoka Wizara ya Biashara;

(vi) Katibu Mkuu, kutoka Wizara ya Fedha;

(vii) Rais kutoka jumuiya wa wafanyabiashara, wenye viwanda na wakulima;

(viii) Mwenyekiti wa makampuni ya Bakheresa;

(ix) Katibu Mtendaji kutoka Tume ya Mipango;

(x) Mkurugenzi Mtendaji kutoka mamlaka ya ukuzaji uwekezaji –Zanzibar;

(xi) Kamishina wa Mmlaka ya kodi ya mapato – Tanzania;

(xii) Kamishina wa Bodi ya Mapato-Zanzibar; na

(xiii) Mjumbe kutoka jumuiya ya usafirishaji na utoaji mizigo;

(b) Wajumbe wa Kamati ya Utalii

(i) Waziri mwenye dhamana na Utalii ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu;

(iii) Waziri wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(iv) Waziri kutoka Afisi ya Makamu wa Pili;

(v) Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi;

(vi) Katibu Mkuu, Wizara ya Utalii;

(vii) Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii;

(viii) Mkurugenzi Mtendaji kutoka mamlaka ya ukuzaji uwekezaji –Zanzibar;

(ix) Mjumbe kutoka Jumuiya ya Utalii na Uwekezaji; na

(x) Mjumbe kutoka Jumuiya ya wanaotembeza watalii;

(c) Kamati ya Kilimo ,Ufugaji na Uvuvi

(i) Waziri wa Kilimo ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri wa Biashara;

(iii) Waziri wa Ardhi;

(iv) Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo;

(v) Mjumbe kutoka Jumuiya wa wakulima wa Karafuu;

(vi) Mjummbe kutoka Jumuiya wa wafanyabiashara, wenye viwanda na wakulima;

(vii) Mkuu wa Taasisi ya utafiti wa kilimo-Zanzibar;

(viii) Mjumbe kutoka Chama cha wakulima wa matunda na mboga mboga-Zanzibar; na

(ix) Mjumbe kutoka chama cha wafugaji - Zanzibar.

(d) Wajumbe wa Kamati ya masuali yanayohusian na Ajira

(i) Waziri wa Ajira ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri wa Utumishi wa Umma;

(iii) Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi;

(iv) Katibu Mkuu, Wizara ya Utumishi wa Umma;

(v) Mjumbe kutoka Chama cha Wakandarasi;

(vi) Kamishna wa Kazi;

(vii) Kamishina wa Uhamiaji-Zanzibar;

(viii) Mjumbe kutoka Chama cha Waajiri - Zanzibar;

(ix) Mjumbe kutoka Chama cha Wafanyakazi-Zanzibar; na

(x) Mkuu wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu ya Mswada huu ni kuanzisha Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara ambayo imeanzisha Baraza na kutoa mambo mengine yanayohusiana na hayo. Baraza litakuwa na wajibu wa kuratibu jukwaa la mazungumzo ya kibiashara baina ya sekta za umma na sekta binafsi. Mswaada unaopendekezwa unakusudia kuimarisha mfumo wa kisheria ambao utaliwezesha Baraza kusimamia ipasavyo kuzingatia na kujadili mambo yote ya kibiashara yatokanayo la jukwaa la kibiashara kwa utaratibu mzuri.

Vilevile, Baraza la Taifa la Biashara linalopendekezwa litahakikisha kwamba sera ya mahusiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi inatekelezwa ipasavyo kwa ajili ya kuhakikisha maslahi ya pande zote mbili husika yanaimarishwa na maendeleo ya kijamiii na kiuchumi na kibiashara-Zanzibar yanaimarishwa.

Mswada una malengo ya kuondosha vikwazo vya kibiashara ambavyo si vya lazima katika uendeshaji wa biashara. Kwa muktadha huo, inaanzisha utaratibu wa kisheria ambao utawajumuisha sekta za umma na sekta binafsi kwa ajili ya kujadili na kutafuta suluhisho la matatizo na vikwazo vya kibiashara na kuhakikisha uendeshaji ulio bora na kukuza ustawi wa jamii ya Zanzibari.

Baraza la Taifa la Biashara litatekeleza kazi zake chini ya maelekezo ya Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara kwa upande mmoja na wajumbe walioteuliwa kutoka Baraza la Mapinduzi na kwa upande wa pili wajumbe kutoka sekta binafsi .Baraza litakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atakuwa na wajibu wa kuhakikisha maelekezo, miongozo na maazimio ya Baraza yanatekelezwa kwa ubora na ufanisi.

Vilevile, Mswada unaopendekezwa unaanzisha kamati tendaji ambayo itajumuisha wataalamu kutoka Serikalini na sekta binafsi ambayo itawajibika kwa Baraza, Kamati tendaji itakuwa ni chombo muhimu sana katika utekelezaji wa kazi za Baraza.

Mswada, vilevile unaanzisha kamati mbalimbali, miongoni mwa kamati hizo ni kamati ya uchumi, biashara, uwekezaji na kodi, kamati ya utalii na kamati nyenginezo zinazofanana na hizo kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Baraza. Pia, Baraza limepewa uwezo kwa kupunguza au kuongeza idadi ya kamati kama itakavyoona inafaa, muda baada ya muda

Mswada unapendekezwa kuanzishwa Baraza la biashara kwa kila Mkoa ambayo yatakuwa chini ya uwenyeviti wa Wakuu wa Mkoa husika, Baraza la biashara kwa kila Mkoa husika yatachukuliwa kama kuiunganishi cha kujadili na kuyapatia ufumbuzi masuali ya kibiashara katika ngazi ya Mkoa husika na kuhakiisha maazimio ya Baraza la Taifa la Biashara yanatekelezwa ipasavyo katika ngazi za Mkoa.

Kwa muuktadha huu, Baraza la biashara la Mkoa lililoanzishwa litaonesha vipaumbele vya Taifa kwa kutekeleza sera ya ungatuzi kwa lengo la kuhakikisha huduma bora za kibiashara zinafikiwa na Wananchi na jamii iliyo ukingoni.

Mswada umegawika sehemu kuu nane na kila sehemu imebeba maudhui yenye kujitegemea.

Sehemu ya kwanza inaelezea masharti ya awali ambayo yamejumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika kwenye mswada huu

Sehemu ya pili inahusiana na uanzishwaji wa Baraza, muundo wa wajumbe wa Baraza, kazi na uwezo aliopewa mwenyekiti wa kumteuwa Katibu Mtendaji baada ya kuzingatia sifa zilizopendekezwa katika mswada huu, Katibu Mtendaji atakuwa ni Afisa masuuli wa Baraza na atasimamia kazi za kila siku za Baraza, kwa muktadha huu ufanisi wa usimamizi wa shughuli za Braza utafikiwa.

Sehemu ya tatu inaelezea uanzishwaji wa kamati tendaji, kazi na muundo wa wajumbe wake, utaratibu wa uendeshaji vikao vya kamati umeelezewa katika sehemu hii kama ilivyofafanuliwa kwenye Jadweli la pili la Mswada huu.

Sehemu ya nne inazungumzia uanzishwaji wa kamati mbalimbali za Baraza kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi, miongozo na maazimio ya Baraza yanatekelezwa, mbali na hayo, kamati ambazo zimependekezwa katika mswada huu, Baraza lina uwezo wa kupunguza au kuzidisha idadi ya kamati kama itakavyoona inafaa.

Sehemu ya tano inahusu uanzishwaji wa Baraza la biashara la kila Mkoa, kazi na wajibu wa Mabaraza hayo pamoja na nafasi za Mabaraza hayo katika kuunganisha mtandao wa utendaji kazi kati ya Mabaraza ya biashara ya kila mkoa na Baraza la Taifa la Biashara kwa ajili ya kusikiliza malalamiko na kuyatolea mapendekezo. Mabaraza yatahakikisha yanasaidia maazimio ya Baraza la Taifa la Biashara yanatekelezwa ipasavyo katika ngazi za Mkoa.

Sehemu ya sita inaelezea kuanzishwa kwa jukwaa la majadiliano ya kibiashara, muundo wake na uwezo wa kualika mtu yeyote kuhudhuria katika vikao vyake kwa lengo la kutoa utaalamu na kujibu baadhi ya masuali yatakayoulizwa katika majadiliano hayo.

Sehemu ya saba inaelezea masharti ya fedha ambayo yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Baraza, ripoti za miamala ya fedha, ukaguzi wa fedha na utaratibu wa usimamizi wa miamala ya fedha kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa fedha za Umma na Kanuni zake

Sehemu ya nane inaelezea masharti mengineyo ambayo yanajumuisha uwezo wa Waziri wa kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji ulio bora wa Sheria hii,kufutwa na kubakizwa tangazo la kisheria Nam. 106 of 2011 na mwisho wa sehemu hii ya mswada huu umeambatanishwa na Jadweli la tatu.

ZANZIBAR
20 Aprili, 2017

(MHE. BALOZI. AMINA SALUM ALI)
Waziri wa Biashara, Viwanda
na Masoko Zanzibar

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI YA ZANZIBAR - 2017